TANGAZO LA SERIKALI NA. 186 la tarehe 17/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MIPANGO MIJI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA AMANI YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mipango Miji ya Kurasimisha Makazi yasiyopangwa Eneo la Amani ya mwaka, 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililobainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika Eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na kina katika eneo la kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba AM1 yenye majira - nukta 569819MS, 8809460KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $74^0$ 38'49'' kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba AM2 yenye majira - nukta 569453MS, 8809561KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $15^0$ 34'11'' kwa

*Tangazo la Serikali Na. 186 ( linaendelea)*

umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba AM3 yenye majira - nukta 569358MS, 8809903KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini katika uelekeo wa $01^0$ 01’30’’kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba AM4 yenye majira - nukta 569348MS, 8810435KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa $79^0$478’27’’kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba AM5 yenye majira - nukta 569795MS, 8810516KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $26^0$ 29’54’’ kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba AM6 yenye majira - nukta 569976MS, 8810155KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $22^0$ 23’56’’ kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba AM7 yenye majira - nukta 570177MS, 8809665KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $60^0$ 16’24’’ kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi ulipoanzia.”

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*